# Serikali yapata ufumbuzi changamoto mazao ya uvuvi

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega (Mb) ameupongeza Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kwa kuyafanyia kazi maono ya serikali ya kuhifadhi mazao ya uvuvi ambayo yamekuwa yakiharibika kutokana na kukosekana kwa nyenzo za kuyahifadhi.

Naibu Waziri Ulega amebainisha hayo mwishoni mwa wiki akiwa katika Kijiji cha Songosongo kilichopo Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa na WWF kwa ufadhili wa Climateworks Foundation chenye thamani ya Shilingi Milioni 424, kwa ajili ya kuhifadhia samaki wanaovuliwa na wanakijiji hao.

Alisema, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/22 imeweka mipango mbalimbali ya kuhakikisha inaongeza vituo vya kuhifadhia mazao ya uvuvi ili wavuvi waondokane na changamoto ya samaki kuharibika kutokana na ukosefu wa barafu na maeneo ya kuyahifadhia mazao hayo.

"Hali duni inachangiwa na upotevu wa mazao wanayovua kutokana na uvuvi na pia kutokuwa na uhakika wa masoko ya mazao wanayoyapata ndiyo maana serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inakuja na suluhu kuokoa wavuvi na watanzania kwa ujumla wake." alisema Ulega.

Aidha, katika kuhakikisha mazao ya uvuvi yanakuwa na masoko ya uhakika Ulega amesema azma ya wizara hiyo ni kuona mazao hayo yanasimamiwa na ushirika hali ambayo itasaidia kuwa na umoja ambao utawezesha wavuvi kusikilizwa na kupata masoko kwa pamoja.

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakuja na mkakati wa usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya vichanja maalum kwa ajili ya kukaushia dagaa na samaki ili kuzuia mazao hayo kutokuwa na mchanga na kuyaongezea thamani kwa kupata masoko zaidi ndani na nje ya nchi hali itakayobadilisha uchumi wa wavuvi na serikali kupata mapato zaidi.

Kuhusu zao la mwani ambalo wanakijiji cha Songosongo wamelalamikia kukosa masoko hali inayosababisha nyumba zao kurundikana zao hilo na hatimaye kuharibika na wakati mwingine kuuza kwa bei ndogo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega amesema katika kipindi hiki wizara itapitia upya sheria inayosimamia zao la mwani ili kubaini changamoto ambazo ni kero kwa wafanyabiashara wa zao hilo na kuziondoa ili wakulima wa mwani na wafanyabiashara waweze kunufaika.

"Moja ya jambo ambalo pamoja na kutafuta soko la mwani tutengeneze kiwanda kidogo cha kukausha mwani na kuliongezea thamani zao hilo ili wakulima waweze kuhifadhi vizuri mwani na kuuza kwa bei nzuri zaidi kuelekea katika uchumi wa bluu," alifafanua Ulega.

Aliongeza kuwa kupitia zao la mwani wanakijiji cha Songosongo wataweza kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na mwani ikiwemo sabuni na kuuomba Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kufikisha elimu ya ujasiriamali kwa wanakijiji hao juu ya masuala ya ujasiriamali.

Aidha, Naibu Waziri Ulega alisema ni wakati muafaka kwa serikali kuangalia upya Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) badala ya kulinda rasilimali za uvuvi pekee viweze kunufaika kwa kupata mikopo na kuendesha shughuli zao.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa WWF Tanzania, Dk. Amani Ngusaru alisema kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa katika Kijiji cha Songosongo Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi chini ya ufadhili wa Climateworks Foundation chenye thamani ya Shilingi Milioni 424, kina uwezo wa kuzalisha barafu Tani 1.4 kwa saa 24.

Dk. Ngusaru alisema mradi huo umeenda sambamba na uhamasishaji wa ufungaji wa miamba ya samaki aina ya pweza ambapo inakadiriwa kwa kipindi cha miaka mwili ya mradi, Tani 91,000 za pweza zimevuliwa katika Kijiji cha Songosongo zenye thamani ya Shilingi Milioni 458, ambapo fedha hizo zimetokana na ufungaji wa miamba kwa awamu tano.

Aliongeza kuwa kuhusu changamoto za zao la mwani anaanza kulifanyia kazi kwa kuwasiliana na makao makuu ya WWF ili kupata namna bora ya wakulima wa zao la mwani hapa nchini wakiwemo wa Kijiji cha Songosongo kuwa na masoko ya uhakika ya zao hilo.

Aidha, kuhusu kilio cha kukosekana kwa boti ya doria kwa ajili kikundi cha BMU katika Kijiji cha Songosongo, Dk. Ngusaru amesema WWF imepokea kilio hicho na kuahidi kuleta boti na injini yake ili kurahisisha shughuli za doria katika maeneo ya miamba ya uzalishaji wa samaki aina ya Pweza.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TAFIRI), Dk. Ishmael Kimirei alisema ili kuhakikisha kituo cha uzalishaji barafu kilichopo katika Kijiji cha Songosongo kinakuwa na tija ni lazima uvuaji wa samaki aina ya pweza uwe endelevu na kuhakikisha upotevu wa samaki hao unapunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Dk. Kimirei alitolea mfano wa moja ya mitambo ya uzalishaji barafu iliyowekwa katika mwambao wa Ziwa Tanganyika lakini wavuvi wakafikiri barafu zinaharibu samaki na hawakutaka kuutumia, lakini wavuvi hao walipokuja kugundua faida ya barafu hivi sasa mahitaji ya barafu hayatoshi.

Alifafanua kuwa mitambo hiyo ni muhimu na imetumia fedha nyingi hivyo wanakijiji cha Songosongo waweze kutumia kwa namna ambavyo imepangwa kutumiwa na kuitunza mitambo hiyo kwa ajili ya uhifadhi wa samaki aina ya pweza pamoja na samaki wengine.

Nao baadhi ya wanakijiji cha Songosongo wamesema wamefurahishwa na kuwepo kwa kituo hicho cha kuzalisha barafu hali ambayo itawasaidia kuzalisha barafu kwa wingi na kutunza samaki ili wasiharibike na kuiomba serikali pamoja na WWF kuangalia namna ya kuwasaidia waweze kunufaika na zao la mwani kwa kuwa kwa sasa wafanyabiashara wengi wanashindwa kwenda kununua kutokana na gharama za ushuru hali inayosababisha wakulima wa zao hilo kufikia kuuza Kilogramu Moja ya mwani kwa Shilingi 400.

Scanned with CamScanner

# *Waziri Ndaki afurahishwa na mafanikio ya BRELA*

**NA MWANDISHI WETU, MWANZA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amefurahishwa na hatua iliyofikiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kupunguza urasimu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa maonyesho ya ya Biashara, Uwekezaji na Utalii, katika viwanja vya Rock City Mall jijini hapa.

Alielezea kufurahishwa na hatua hiyo baada ya kupewa ufafanuzi na Ofisa Usajili kutoka BRELA, Gabriel Girangay kuhusu jitihada zilizofanyika kumaliza tatizo hilo alipotembelea Banda la maonesho la BRELA

Girangay alisema BRELA imeboresha huduma inazotoa kwa wadau wake ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kukamilisha usajili kwa kadri inavyowezekana lakini pia kuwahudumia wateja wote kwa ukaribu kupitia kituo cha miito.

"Kwa sasa muda wa usajili wa Jina la biashara ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi, Usajili wa kampuni ni siku tatu (3) na si zaidi ya siku tano (5) za kazi. Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku tisini (90) (kutokana na takwa la kisheria)," alisema.

"Maombi ya kupata Hataza ni siku mia moja na ishirini (120) (kutokana na takwa la kisheria), kupata Leseni ya Kiwanda au Leseni ya Biashara kundi A ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi," alisema.

Akizungumza kenye ufunguzi wa maonesho hayo, Ndaki amewataka wafanyabiashara na wajasiriamali wa Mkoa wa Mwaza kutumia fursa ya uwepo wa BRELA katika maonesho haya kutatua changamoto zao na kupata elimu.

"Changamoto zinazosemekana zipo katika urasimishaji biashara sasa ndio muda wake kuzimaliza na bahati nzuri BRELA wapo katika maonesho haya, fikeni katika banda lao la maonesho, pateni elimu, wasilisheni changamoto zenu hapo na rasimisheni biashara papo kwa hapo," alisema Ndaki.

Girangay alisema BRELA inashiriki maonesho haya ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kuwafikia wadau wake katika maeneo yao kwa lengo la kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara.

Alisema wanaelimisha pia kuhusu, taratibu za urasimishaji biashara na gharama zake, kutatua changamoto na kufanya usajili wa papo kwa hapo.

Maonesho ya Biashara Uwekezaji yaliyoandaliwa na Rock City Mall yanafanyika kwa siku tatu yalianza Aprili 30 na yanatarajiwa kumalizika leo Jumapili.

Tanzanite uk. 3, 03/05/2021

Scanned with CamScanner

## hamani ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha barafu

# Naibu Waziri Ulega 'aipa tano' WWF kuyafanyia kazi maono ya serikali

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameupongeza Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kwa kuyafanyia kazi maono ya serikali ya kuhifadhi mazao ya uvuvi, ambayo yamekuwa yakiharibika kutokana na kukosekana kwa nyenzo za kuyahifadhi.

Ulega, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, akiwa katika Kijiji cha Songosongo, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wakati wa hafla ya kukabidhi kituo cha kuzalisha barafu, kilichojengwa na WWF kwa ufadhili wa Climateworks Foundation, chenye thamani ya sh. milioni 424, kwa ajili ya kuhifadhia samaki wanaovuliwa na wanakijiji hao.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2021/22, imeweka mipango mbalimbali ya kuhakikisha inaongeza vituo vya kuhifadhia mazao ya uvuvi, ili wavuvi waondokane na changamoto ya samaki kuharibika kutokana na ukosefu wa barafu na maeneo ya kuyahifadhia mazao hayo.

"Hali duni inachangiwa na upotevu wa mazao wanayovua kutokana na uvuvi, na pia kutokuwa na uhakika wa masoko ya mazao wanayoyapata, ndiyo maana serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inakuja na suluhu kuokoa wavuvi na Watanzania kwa ujumla wake," alisema.

Katika kuhakikisha mazao ya uvuvi yanakuwa na masoko ya uhakika, Naibu Waziri Ulega, alisema azma ya wizara hiyo ni kuona mazao hayo yanasimamiwa na ushirika ili kusaidia kuwa na umoja, ambao utawawezesha wavuvi kusikilizwa na kupata masoko kwa pamoja.

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi, itakuja na mkakati wa usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya vichanja maalumu kwa ajili ya kukaushia dagaa na samaki, ili kuzuia mazao hayo kutokuwa na mchanga na kuyaongezea thamani kwa kupata masoko zaidi ndani na nje ya nchi, hali itakayobadilisha uchumi wa wavuvi na serikali kupata mapato zaidi.

Kuhusu zao la mwani, ambalo wanakijiji wa Songosongo wamelalamikia kukosa masoko, hali inayosababisha nyumba zao kurundikana zao hilo na hatimaye kuharibika na wakati mwingine kuuza kwa bei ndogo, Ulega alisema wizara itapitia upya sheria inayosimamia zao hilo ili kubaini changamoto ambazo ni kero kwa wafanyabiashara.

"Pamoja na kutafuta soko la mwani, tutatengeneza kiwanda kidogo cha kukausha mwani na kuliongezea thamani zao hilo, ili wakulima waweze kuhifadhi vizuri mwani na kuuza kwa bei nzuri zaidi kuelekea katika uchumi wa buluu," alisema.


Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa WWF Tanzania, Dk. Amani Ngusaru, alisema kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa katika Kijiji cha Songosongo, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, chini ya ufadhili wa Climateworks Foundation, kina uwezo wa kuzalisha barafu tani 1.4, kwa saa 24.

Dk. Ngusaru, alisema mradi huo umeenda sambamba na uhamasishaji wa ufungaji wa miamba ya samaki aina ya pweza, ambapo inakadiriwa kwa kipindi cha miaka mwili ya mradi, tani 91,000, za pweza zimevuliwa katika Kijiji cha Songosongo, wenye thamani ya sh. milioni 458, ambapo fedha hizo zimetokana na ufungaji wa miamba kwa awamu tano.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TAFIRI), Dk. Ishmael Kimirei, alisema ili kituo cha uzalishaji barafu kiwe na tija, lazima uvuaji wa samaki aina ya pweza uwe endelevu na kuhakikisha upotevu wa samaki hao unapunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Dk. Kimirei, alitolea mfano wa moja ya mitambo ya uzalishaji barafu, iliyowekwa katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, wavuvi wakafikiri barafu zinaharibu samaki na hawakutaka kuutumia, lakini walipokuja kugundua faida yake, mahitaji hivi sasa ni makubwa zaidi.

MAZUNGUMZO



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Songosongo, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wakati wa kukabidhi kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF). (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner

# Waziri afurahia Brela kupunguza urasimu

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

WAZIRI+ wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amefurahishwa na hatua iliyofikiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kupunguza urasimu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Maonesho ya Biashara, Uwekezaji na Utalii katika viwanja vya Rock City Mall jijini hapa.

Alielezea kufurahishwa na hatua hiyo baada ya kupewa ufafanuzi na Ofisa Usajili kutoka Brela, Gabriel Girangay kuhusu jitihada zilizofanyika kumaliza tatizo hilo alipotembelea Banda la Brela.

Girangay alisema Brela imeboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kukamilisha usajili kwa kadri inavyowezekana, pia kuwahudumia wateja wote kwa ukaribu kupitia kituo cha miito.

"Kwa sasa muda wa usajili wa jina la biashara ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi, usajili wa kampuni ni siku tatu na si zaidi ya siku tano za kazi. Usajili wa alama za biashara na huduma ni kipindi cha siku 90 kutokana na takwa la kisheria," alisema.

Akaongeza: "Maombi ya kupata ni siku 120 kutokana na takwa la kisheria, kupata leseni ya kiwanda au leseni ya biashara kundi A ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi."

Girangay alisema Brela inashiriki maonesho haya ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kuwafikia wadau wake katika maeneo yao ili kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara.

Katika ufunguzi wa maonesho hayo, Waziri Ndaki aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali wa Mkoa wa Mwaza kutumia fursa ya uwepo wa Brela katika maonesho haya kutatua changamoto zao na kupata elimu.

Habari Leo uk. 17, 03/05/2021

Scanned with CamScanner

# Changamoto ya upotevu wa mazao ya uvuvi yaanza kupatiwa majibu

**Na Edward Kondela**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (Mb) ameupongeza Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kwa kuyafanyia kazi maono ya serikali ya kuhifadhi mazao ya uvuvi ambayo yamekuwa yakiharibika kutokana na kukosekana kwa nyenzo za kuyahifadhi.

Naibu Waziri Ulega alibainisha hayo juzi akiwa katika Kijiji cha Songosongo kilichopo Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa na WWF kwa ufadhili wa Climateworks Foundation chenye thamani ya Shilingi Milioni 424, kwa ajili ya kuhifadhia samaki wanaovuliwa na wanakijiji hao.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/22 imeweka mipango mbalimbali ya kuhakikisha inaongeza vituo vya kuhifadhia mazao ya uvuvi ili wavuvi waondokane na changamoto ya samaki kuharibika kutokana na ukosefu wa barafu na maeneo ya kuyahifadhia mazao hayo.

"Hali duni inachangiwa na upotevu wa mazao wanayovua kutokana na uvuvi na pia kutokuwa na uhakika wa masoko ya mazao wanayoyapata ndiyo maana serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inakuja na suluhu kuokoa wavuvi na watanzania kwa ujumla wake," alisema Ulega.

Aidha,katika kuhakikisha mazao ya uvuvi yanakuwa na masoko ya uhakika Ulega alisema azma ya wizara hiyo ni kuona mazao hayo yanasimamiwa na ushirika hali ambayo itasaidia kuwa na umoja ambao utawezesha wavuvi kusikilizwa na kupata masoko kwa pamoja.

Pia alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakuja na mkakati wa usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya vichanja maalum kwa ajili ya kukaushia dagaa na samaki ili kuzuia mazao hayo kutokuwa na mchanga na kuyaongezea thamani kwa kupata masoko zaidi ndani na nje ya nchi hali itakayobadilisha uchumi wa wavuvi na serikali kupata mapato zaidi.

Kuhusu zao la mwani ambalo wanakijiji cha Songosongo wamelalamikia kukosa masoko hali inayosababisha nyumba zao kurundikana zao hilo na hatimaye kuharibika na wakati mwingine kuuza kwa bei ndogo, Naibu Ulega alisema katika kipindi hiki wizara itapitia upya sheria inayosimamia zao la mwani ili kubaini changamoto ambazo ni kero kwa wafanyabiashara wa zao hilo na kuziondoa ili wakulima wa mwani na wafanyabiashara waweze kunufaika.

"Moja ya jambo ambalo pamoja na kutafuta soko la mwani tutengeneze kiwanda kidogo cha kukausha mwani na kuliongezea thamani zao hilo ili wakulima waweze kuhifadhi vizuri mwani na kuuza kwa bei nzuri zaidi kuelekea katika uchumi wa bluu," alifafanua Ulega.

Aliongeza kuwa kupitia zao la mwani wanakijiji cha Songosongo wataweza kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na mwani ikiwemo sabuni na kuuomba Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kufikisha elimu ya ujasiriamali kwa wanakijiji hao juu ya masuala ya ujasiriamali.

Naibu Waziri Ulega pia alisema ni wakati muafaka kwa Serikali kuangalia upya Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) badala ya kulinda rasilimali za uvuvi pekee viweze kunufaika kwa kupata mikopo na kuendesha shughuli zao.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa WWF Tanzania Dkt. Amani Ngusaru alisema kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa katika Kijiji cha Songosongo Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi chini ya ufadhili wa Climateworks Foundation chenye thamani ya Shilingi Milioni 424, kina uwezo wa kuzalisha barafu Tani 1.4 kwa saa 24.

Dkt Ngusaru alisema mradi huo umeenda sambamba na uhamasishaji wa ufungaji wa miamba ya samaki aina ya pweza ambapo inakadiriwa kwa kipindi cha miaka mwili ya mradi, Tani 91,000 za pweza zimevuliwa katika Kijiji cha Songosongo zenye thamani ya Shilingi Milioni 458, ambapo fedha hizo zimetokana na ufungaji wa miamba kwa awamu tano.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TAFIRI) Dkt. Ishmael Kimirei alisema ili kuhakikisha kituo cha uzalishaji barafu kilichopo katika Kijiji cha Songosongo kinakuwa na tija ni lazima uvuaji wa samaki aina ya pweza uwe endelevu na kuhakikisha upotevu wa samaki hao unapunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Dkt Kimirei alitolea mfano wa moja ya mitambo ya uzalishaji barafu iliyowekwa katika mwambao wa Ziwa Tanganyika lakini wavuvi wakafikiri barafu zinaharibu samaki na hawakutaka kuutumia, lakini wavuvi hao walipokuja kugundua faida ya barafu hivi sasa mahitaji ya barafu hayatoshi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na wanakijiji wa Songosongo wilayani Kilwa mkoani Lindi wakati wa hafla fupi ya kukabidhi kituo cha kuzalisha barafu kilichojengwa na Mfuko wa Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), kwa ufadhili wa Climateworks Foundation, ambapo aliwapongeza WWF kwa kufanyia kazi maono ya serikali ya kuhifadhi mazao ya uvuvi, ambayo imekuwa huharibika kutokana na kukosekana kwa nyenzo za kuhifadhi, ikiwemo barafu. (Picha na Edward Kondela, Afisa Habari – Wizara ya Mifugo na Uvuvi)

Scanned with CamScanner

Uk. 11



# Waziri Ndaki afurahishwa na mafanikio ya BRELA

Na Mwandishi Wetu, Mwanza

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amefurahishwa na hatua iliyofikiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kupunguza urasimu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa maonesho ya Biashara, Uwekezaji na Utalii, katika viwanja vya Rock City Mall jijini hapa.

Aliekezea kufurahishwa na hatua hiyo baada ya kupewa ufafanuzi na Ofisa Usajili kutoka BRELA, Gabriel Girangay kuhusu jithada zilizofanyika kumaliza tatizo hilo alipotembelea Banda la maonesho la BRELA.

Girangay alisema BRELA imeboresha huduma inazotoa kwa wadau wake ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kukamilisha usajili kwa kadri inavyowezekana lakini pia kuwahudumia wateja wote kwa ukaribu kupitia kituo cha mito.

"Kwa sasa muda wa usajili wa jina la biashara ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi, usajili wa kampuni ni siku tatu na si zaidi ya siku tano za kazi.

Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku tisini kutokana na takwa la kisheria," alisema.

"Maombi ya kupata Hataza ni siku 120 kutokana na takwa la kisheria, kupata leseni ya Kwanda au Leseni ya Biashara kundi A ni siku moja na si zaidi ya siku tatu za kazi," alisema.

Akizungumza kenye ufunguzi wa maonesho hayo, Ndaki aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali wa Mkoa wa Mwaza kutumia fursa ya uwepo wa BRELA katika maonesho haya kutatua changamoto zao na kupata elimu.

"Changamoto zinazosemekana zipo katika urasimishaji biashara sasa ndio muda wake kuzimaliza na bahati nzuri BRELA wapo katika maonesho haya, fikeni katika banda lao la maonesho, pateni elimu, wasilisheni changamoto zenu hapo na rasimisheni biashara papo kwa hapo," alisema Ndaki.

Girangay alisema BRELA inashiriki maonesho haya ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kuwafikia wadau wake katika maeneo yao kwa lengo la kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara.

Alisema wanaelimisha pia kuhusu, taratibu za urasimishaji biashara na gharama zake, kutatua changamoto na kufanya usajili wa papo kwa hapo.

Maonesho ya Biashara Uwekezaji yaliyoandaliwa na Rock City Mall yanafanyika kwa siku tatu yalianza Aprili 30 na yanatarajiwa kumalizika leo Jumapili.

MWANANCHI.CO.TZ JUMATATU, MEI 3, 2021

# Mkirikiti ahamasisha elimu kwa wafugaji

**Simanjiro.** Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti amepongeza jamii ya wafugaji wa Wilaya ya Simanjiro kuweka kipaumbele kwenye elimu na kuhakikisha watoto wao wanakwenda shule.

Mkirikiti aliyasema hayo juzi wakati akikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa madarasa na vyoo katika shule ya Msingi Losokonoi wilayani Simanjiro.

Alisema wanafunzi wa jamii ya wafugaji wa wilaya ya hiyo hivi sasa wanaona elimu ni kipaumbele japokuwa wengi wao hutembea umbali mrefu kwenda shule.

Alimpongeza mwalimu mkuu wa shule hiyo kwa ufaulu mzuri wa darasa la saba na akaagiza mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo, Yefred Myenzi na mwenyekiti wake Baraka Kanunga wampe zawadi ya mbuzi.

Kati ya watoto 17 waliofanya mtihani 14 walichaguliwa kwenda sekondari. **(Joseph Lyimo)**

Scanned with CamScanner